LEARNING BY EAR - Girls
5th EPISODE
Sexual Abuse Part 2
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

CHARACTERS:
Anchor: …Intro/Outro
BIBIY......Main Character.
SAMERAS MOTHER.......Same as in Part 1
BAMU....Sameras Uncle........Same as in Part 1.
VILLAGE CHIEF..........Male.......(Adult)
ALMA...Same Character

Intro:
Ni wakati mwingine tena tunapokutana kwenye mfululizo wa mchezo wa kuigiza unao kujia kila wiki katika makala ya Jifunze Kwa Kusikiliza. Wiki iliyopita tulilisikiliza sehemu ya kwanza ya kisa Udhalilishaji wa Kingono dhidi ya wasichana. Samera amenasa kwenye mtego wa mjomba wake Bamu. Bibiy nae ameapa kuwa mjomba Bamu atakiona cha mtema kuni. Je ni yapi yatakayotokea baada ya Bamu kujulikana kuwa ndie mwenye mzigo wa Samera? Karibu kwenye sehemu ya tano ya mchezo wa kuigiza ambapo leo tutasikiliza sehemu ya pili ya kisa Udhalilishaji wa Kingono.

Sign Tune

SCENE ONE:
(Bibiy anazungumza na wasichana wenzake akiwashawishi wajiunge katika kampeni ya kuwaokoa watoto wanaokabiliwa na hali ngumu katika uwanja wa shule keleel za wanafunzi zinasikika)
(African Drums)

BIBIY: Rafiki zangu nimewaita hapa ili niwaambieni habari mbaya kuhusu rafiki yetu Samera. Hivi tunavyozungumza mwenzetu yuko hospitali, alipelekwa baada ya kuugua, na

habari mbaya ni kwamba Samera ni mja mzito yaani ana mimba..ndio maana nataka tuungane pamoja ili tumsaidie rafiki yetu huyu.

ALMA: Eti unasemaje Bibiy! Samera ana mimba? Imekuwaje mimi hata sielewi mbona ana miaka15 tu..Eti Samera ana mimba unasema kweli Bibiy?

BIBIY: Ni kweli Alma hayo ninayo yasema.. nilivyo kwenda kumtembelea hospitalini Samera alinieleza kila kitu.. aliniambia kuwa amedhulumiwa na mjomba wake tu!.. yaani huyu mjomba wake alikuwa akimdhalilisha kwa muda, mpaka alipopata mimba. Kwa kweli rafiki yetu ana huzuni sana hebu fikiria ikiwa mkasa huu utakupata wewe jamani.

ALMA: Loo hata sitaki kujifananisha.. jamani balaa gani hili kwa nini lakini watu wengine wanakosa imani kabisa? Najaribu kufikiria vile Samera masikini alivyo huzunika.

BIBIY: Yeah! Hata mimi niliwahi kusoma kwenye mtandao kuhusu watoto wanaodhalilishwa, niligundua kwamba hali hiyo inaweza kusabisha madhara makubwa tena ya muda mrefu kwa mtoto. Nyanya yangu pia aliwahi kuniambia wakati fulani kuwa lazima tujaribu kila wakati kuzungumza dhidi ya hali yoyote ile inayomdhalilisha mtoto yaani tukiona tu mtoto, mwenzetu anateswa iwe kwa kupigwa au hata mtoto huyo akiwa anadhulumiwa kiakili au anaachwa na njaa basi mara moja lazima tuseme, nyanya yangu amesema udhalilishaji wa watoto si sahihi, sio vizuri kuwatesa watoto kwa njia yoyote ile na wala sio sisi watoto wa kulaumiwa.

ALMA:Kwa hiyo Bibiy, Unapanga kufanya nini sasa?unadhani rafiki yetu Samera tutamsaidiaje?

BIBIY: Swali zuri sana hilo Alma. Kwa sasa nataka sisi sote twende tukamuone bwana Chifu ili tukamueleze masikitiko yetu halafu nayeye atatuelekeza njia gani ya kufanya kuhusiana na matatizo ya rafiki yetu Samera. Kwa kuwa mimi nafikiria lazima

mjomba wake Samera aadhibiwe au nyinyi wenzangu mnasemaje? (Watoto wote wanaitikia kwa pamoja ..ndio huyu mzee katili lazima aadhibiwe!)

MUSIC:

SCENE 2:
BIBIY: Mheshimiwa bwana chifu kama nilivyo kueleza.. rafiki yetu Samera ameniambia kuwa matatizo yaliyomkuta yamesababishwa na mjomba wake mwenyewe na sisi tumekasirishwa sana na tukio hilo dhidi ya rafiki yetu ndio maana nimekuja hapa kwako na rafiki zangu ili nikueleze kwa sababu tunataka umsaidie rafiki yetu Samera.

CHIEF: Bibiy, Nimeshtushwa sana kusikia hayo uliyonieleza. Ni jambo la kuvunja moyo kabisa kwamba udhalilishaji huo wa kingono umetendeka katika nyumbani tena uhalifu huo umetendwa na mtu ambae anastahili kumlinda mtoto huyo. Kwa kweli lazima hatua za haraka zichukuliwe.

BIBIY: Ndio maana tumekuja kwako bwana Chifu na kukueleza kila kitu.

CHIEF: Umefanya vizuri sana Bibiy pamoja na wenzako nami naahidi kuwa sitapumzika mpaka muhalifu huyo tumtie mbaroni na sheria ifanye kazi yake. mmefanya kazi nzuri sana lazima vijana muwe macho katika kupambana na uhalifu wa aina yoyote dhidi ya watoto. Bibiy nakupongeza sana kwa ujasiri wako hasa pale unapojitolea bila uoga kupambana na mambo mbalimbali yanayowakabili wasichana wenzako. Endeleza juhudi zako na wala usichoke ni vyema kuielimisha jamii umuhimu wa kujiepusha na maonevu dhidi ya watoto.

BIBIY: Bwana Chifu kwa niaba ya wenzangu ambao wako hapo nje wananingojea napenda kukushukuru kwa kuwa umesema utamsaidia rafiki yetu Samera. Basi naomba ruhusa niondoke, lakini kwanza nauliza kama tunaweza kurudi tena ili tupate kujua umefikia wapi?

CHIEF: Hakuna matata Bibiy – unakaribishwa katika ofisi hii wakati wowote. Ofisi ya Chifu ni ofisi ya umma na inawatumikia wananchi wote watoto kwa wakubwa bila ubaguzi kwa hiyo karibu sana Bibiy na wenzako.

BIBIY: Asante sana muheshimiwa.. bye bye.
(Mlango unafungwa na Chifu anajizungumzia pekeyake)

CHIEF: Ooh! Oooh! Aibu gani hii jamani. Kama haya yangekuwa ni maradhi yamewaambukiza watoto wetu tungekuwa tumeshatangaza hali ya hatari, na fedha za kufanya utafiti pia zingepatikana kwa haraka lakini jambo la kusikitisha ni kuwa watoto wanadhalilishwa kila kukichalakini wala halimtii mtu tumbo joto na wala huwasikii watu wakilivalia njuga swala la unyanyasaji watoto. Ajabu kwamba swala la ngono dhidi ya watoto limebakia kuwa ni swala la familia peke yake, sio mahala kwingi utakapo sikia watu wajkilizungumzia kama maswala mengine. Loo lazima tukazane kuleta mabadiliko watoto wana haki ya kulindwa.
(Nje ya ofisi ya Chifu)

BIBIY: Hey wasichana nawaabmia tuna bahati kweli bwana chifu ameahidi kuwa atamchukulia hatua mjomba wake Samera (wasichana wanaruka ruka kwa furaha) - yoouhuuu! Kikundi chetu cha Girl Power kidumu milele- katu hatutorudi nyuma na kuangalia watoto wakiteswa bure bure - never, never!

MUSIC

SCENE THREE:
(Mlango unagongwa).

CHIEF: Yes,ingia ndani .(Mlango unafunguka). Ooh! Mama Samera, karibu sana, tafadhali kaa kwenye kiti.

MOTHER: Asante sana bwana Chifu. Naam nimekuja ili nijue umefikia wapi tangu tulipozungumza juu matatizo yaliyomfika mwanangu Samera? Mpaka sasa kaka yangu Bamu ndio

ameingia mitini haonekani kabisa hata sijamtia machoni na wala sijui yuko wapi ni muda tangu alipotoweka.

CHIEF: Ndio maana nimekuita hapa ofini kwangu, ninataka nikufahamisha juu ya hatua tuliyofikia hadi sasa.

MOTHER: Oh bwana Chifu kwa kweli nina masikitiko makubwa sana kwa nini kaka yangu Bamu akaamua kuniharibia binti yangu? Hii ni dhambi kubwa kabisa katika dunia yetu . (Analia) Samera wangu masikini ana miaka 15 tu, ndio huyo sasa ana mimba tena mimba yenyewe ya mjomba wake..mbona hii ni aibu kubwa jamani loo..hayasemeki hata kidogo!

CHIEF: Mama Samera, napenda kukufahamisha kuwa hatimaye kaka yako Bamu amekamatwa na hivi sasa yuko kwenye mikono ya polisi amewekwa korokoroni. Yule msichana jasiri Bibiy, si unamjua Yule msichana mwenye nywele za kusokota basi yeye na wenzake wametusaidia sana hadi kumkamata Bamu. Tangu alipofikisha ripoti hapa kwangu, Bibiy hakupumzika hadi tukafanikiwa kumkamata Bamu.

MOTHER: namshukuru sana binti huyo..Lo! bwana Chifu ikiwa kuna mtu niliyemuamini kwa moyo wangu wote basi ni huyo ndugu yangu Bamu lakini amenitenda kisa ambacho sitweza kukisahau maishani mwangu. Hebu fikiria chifu mwanangu ataitwa mama ilihali na yeye bado ni mtoto?, isitoshe mwanangu pia anaweza kupata matatizo mengine (Analia). Hata sijui kama Samera amenusurika magonjwa ya zinaa au hata virusi vya HIV? Nina wasiwasi mwingi sijui daktari atasemaje majibu yatakapotoka..Aah Bamu wee mbona umenidunga mkuki moyoni?

CHIEF: Piga moyo konde Mama Samera –nakuhakiishia kuwa haki lazima itendeke. Ulimwengu wetu wa leo hauna nafasi ya wahalifu wanaowadhulumu watoto, tukiwajua tu lazima wafikishwe mbele ya sheria. Kwa hivyo huyo Bamu ataadhibiwa na tutahakikisha kuwa anagharamia mzigo aliousababisha.

MOTHER: Ndio bwana chifu nataka alazimishwe kulipa gharama zote za hospitali hadi mtoto atakapozaliwa na baadae pia alazimishwe kugharamia malezi ya mtoto maanake bwana chifu mimi nataka mwanangu arudi shule aendelee na masomo yake .

CHIEF: Yote hayo yatatekelezwa mama Samera hata kama tutalazimika kuwauza ng'ombe na mbuzi wake wote tutafanya hivyo. Nakuhakikishia kuwa hatutapumzika hadi haki itakapotendeka.

MOTHER: Asante bwana chifu nimefurahi kusikia kuwa Bamu yuko polisi . Najua sasa kazi iliyobaki ni ya mahakama. Naam bwana chifu nataka kuondoka sasa kwani inanibidi kwenda kumuona daktari nikapate majibu ya mwanangu na Samera pia ananihitaji, Nina wasiwasi sana juu ya hali ya mwanangu. Ooh! Hata sijui nifanyeje natamani ningemkamata huyo Bamu kwa mikono yangu nikipasue kile kichwa chake!

CHIEF: Mama Samera, hiyo haisaidii kitu. Jambo la muhimu ni kuwa Bamu yuko chini ya sheria kwa hivyo atapata adhabu inayomstahili wewe unahitajika kufuata maagizo ya daktari tu ili mwanao apate nafuu na kumbuka kuwa Samera anahitaji ushauri nasaha kutoka kwa watalaamu.

AFRICAN DRUMS

SCENE FOUR:
(Bibiy na wenzake wako mjini kelele za magari na watu zinasikika.)

ALMA: Enhe jamani leo tunaenda kufanya nini katika internet café? nakuuliza Bibiy? maanake nina hamu ya kutaka kujua.

BIBIY: Si tulikubaliana kuwa leo tutafanya utafiti juu ya kuchagua kazi. Nafikiri tukimaliza masomo kila mmoja wetu angependa kufanya kazi tutamuuliza Yule mtalaamu mtaalamu

atuonyeshe jinsi ya kufanya.. Heee! Nakwambia kikundi chetu cha Girl Power kinazidi kuimarika kila siku. Hadi sasa wasichana wengi tu wameshachangia mada mbali mbali kwenye tovuti yetu na wengine wametuma picha za kupendeza kweli.

ALMA: (Wanacheka) Yeah, Yeah! Kweli picha zinafurahisha kweli tena zinapendeza, kama ile picha iliyotumwa na huyu msihana kutoka.... mmmh... Turkana. Nimefurahishwa sana na vazi lake la kiasili kwanza zile shanga zake zenye rangi tafauti za kupendeza shingoni looo! Zimenifurahisha sana ni picha nzuri kweli kweli.

BIBIY: Ha ta ile picha ya wasichana kutoka Mali pia ni poa kweli wao pia wanapendeza. Na kilichonivutia zaidi ni ripoti yao waliyoandika kuhusu mradi wao wa kusafisha mazingira , unajua wasichana hawa wanakutana mara moja kwa mwezi halafu wanafanya usafi katika eneo Fulani la umma kama vile hospitali, shuleni au hata kusafisha barabara wakati mwingine kwa kweli hiyo ni juhudi inayopaswa kusifiwa! Hata sisi tunaweza kuanzisha mradi kama huo hapa kwetu.

ALMA: kweli hiyo ni juhudi inayopaswa kusifiwa na bila shaka inaleta maendeleo makubwa usafi wa mazingira ni muhimu kwa kila mtu. Natumai hata leo tutapata picha na taarifa nyingi za kupendeza pamoja na wanachama wapya katika kikundi chetu cha Girl-Power.

BIBIY: Hata mimi nafikria hivyo Alma, enheee, vipi wewe umeshafikiria unataka kufanya kazi gani ukimaliza masomo?

ALMA: nakawambia Bibiy kwa sasa mimi nafikiria nataka kuwa mwanasheria kwa sababu nitapata fursa ya kuwatetea watoto wanaodhalilishwa nitakuwa mstari wa mbele kutetea haki zao. Siwezi kusahau kamwe yale yaliyomfika rafiki yetu. Aah Bibiy ulifanya vizuri sana kuongoza harakati ambazo zilimfanya mjomba wake Samera akamatwe. Hongera sana Bibiy, ndio maana mimi nataka kuwa mwanasheria sasa.

BIBIY: Asante Alma kwa kunisifu lakini ukumbuke kuwa ilikuwa juhudi yetu sote, kila mmoja wetu alitoa mchango wa kutosha na yote hayo yaliwezekana kwa kuwa sisi tunashirikiana kwa kila jambo. Inatubidi tuendeleze umoja wetu na ushirikiano wetu ili tupate kupambana na maonevu ya kila aina yanayotendendewa wasichana.

ALMA: Lo yaani ni vigumu sana kuamini kuwa mjomba wako tu anaweza kukufanyia unyama kiasi hicho! Kama rafiki yetu Samera alivyodhulumiwa, Bibiy nakuahidi kila siku nitakuwa msatari wa mbele kutetea maslahi ya wasichana.

BIBIY: Yeah! Alma maonevu mengi tu yanatendewa watoto isipokuwa shida kubwa iliyopo ni kwamba watoto wengi wanapuuza yale wanayoambiwa na wazazi wao. Nyanya yangu mara kwa mara anasema kuwa watoto hawapaswi kupokea zawadi kutoka kwa mtu yeyote bila kuwafahamisha wazazi wao na pia yeye huniambia kila siku kuwa lazima watoto tuwaheshimu watu wakubwa kwa mfano tusiwaite kwa majina yao. Na lazima tuwajulishe wazazi wetu popote pale twendapo. Lakini si unaona kuwa watoto wengi wanapuuza mambo hayo ya muhimu?

ALMA: Ni kweli Bibiy ndio maana ninaomba mjomba wake Samera afungwe jela maisha yake yote ili asiwe karibu na wasichana tena.

BIBIY: Nafahamu una maanisha nini Alma lakini hiyo sasa ni kazi ya mahakama. Muhimu ni kuwa rafiki yetu Samera hatimaye atapata nafuu na kuweza kurudi shule tena. Hey Alma unakumbuka kuwa timu yetu ya wasichana ya mpira wa miguu itashindana na timu ya wavulana wiki ijayo?

ALMA: Wooow! Nakumbuka sana na nimekuwa naisubiri kwa hamu kubwa siku hiyo lazima tuwaonyeshe wavulana kuwa tunaweza kuwafunga mabao mengi tu, kwani wao wanafikiri kuwa sisi hatuwezi kucheza mpira wa miguu. Usisahau kesho tuna mazoezi kwenye uwanja wa shule.

BIBIY: Mimi napenda sana kuwaangalia wasichana wakicheza Football. Inawezekana pia hata siku moja na sisi tutacheza mechi za kimataifa, kila jambo ni kufanya bidii tu.

ALMA: Inawezekana kabisa sisi kucheza mechi za kimataifa, dunia ni watu na watu wenyewe ndio sisi kwa nini isiwezekane? Zamani wanawake walikuwa hawachezi kabisa Football lakini sasa mambo ni mengine. (Wanacheka) Yaani sijui wavulana wataangalia wapi siku hiyo tukiwafunga mabao mawili kwa bila!.

BIBIY: Yeah! Unajua wanasema kila siku kuwa football ni mchezo wa kubahatisha lakini sisi hatutategemea bahati peke yake tutatumia ujuzi na maarifa yaani tutawaonyesha mpira wa kikweli au kabumbu yenyewe.Hey Alma, mimi nitakuacha sasa nataka kupitia kwa dobi nikachukue jezi zetu basi tutaonana baadae!

ALMA: OK, Bob Marley wetu hadi baadae nipe tano basi (wanagonga mikono) Bye!

Autro: Kila la kheri tunawatakia wasichana katika mchuano wa kabumbu kati ya timu yao na timu ya wavulana. Hadi hapo ndio tumefikia mwisho wa makala haya ya Jifunze kwa Kusikiliza kwa leo. Kumbuka kuwa unaweza kuusikiliza tena mchezo huu au pia unaweza kumwambia rafiki ausikilize kupitia kwenye tovuti yetu. HYPERLINK "http://www.dw-world.de/lbe" www.dw-world.de/lbe. Hadi tutakapo kutana tena wiki ijayo kwaheri.

END